## We Move – Mobility Equipment Grant Guidelines (Tunasonga - Miongozo ya Ruzuku ya Vifaa vya Uhamaji)

Ruzuku hii inaweza kununua vifaa vya ulemavu vinavyobadilisha maisha kwa watoto ambavyo havipatikani kwa urahisi kupitia huduma za kawaida.

Mwombaji anaweza kuchagua kipengee kimoja au zaidi, ambacho kinahusiana moja kwa moja na utambuzi (diagnosis) wa mtoto na kikiungwa mkono na GP au mtaalamu wa afya shirikishi.

### Kustahiki

- Watoto wa miaka 0 - 18
- Watoto wenye ulemavu au ugonjwa wa muda mrefu uliyoandikwa rasmi na mtaalamu wa afya anayetambuliwa.
- Jumla ya mapato ya kaya (famiia) ni chini ya $200,000 kwa mwaka (ikijumuisha usaidizi wa watoto, mapato ya uwekezaji, mapato ya ng'ambo, au mapato mengine yoyote)
- Wakazi wote wa NSW na ACT wanakaribishwa kutuma ombi, ikijumuisha watu wasio raia na wenye viza ya muda.

### Mifano ya maombi yanayostahiki

- Vifaa vya kuchezea vinavyobadilika na vifaa vya usalama
- Pramu za mahitaji maalum na viti vyakusuma vya watoto.
- Viti vya magurudumu - lazima vichunguzwe, vielekezwe, na vijaribiwe na OT
- Viti vinavyobadilika na viti maalumu vya gari
- Baiskeli zilizobadilishwa, baiskeli ya magurudumu tatu na pikipiki
- Mbwa wa usaidizi (ufadhili wa sehemu). Inazingatiwa tu ikiwa wanatoa uhamaji na uhuru

### Nyaraka (documents) zinazohitajika

Viambatisho vifuatavyo lazima vijumuishwe kama sehemu ya maombi

1. **Barua ya GP au Daktari wa Watoto** inayoelezea utambuzi (diagnosis)/hali ya mtoto. Lazima iwe na tarehe katika miezi 12 ya maombi
2. **Barua ya usaidizi** kutoka kwa mtaalamu wa afya (kwa mfano, mtaalamu wa tiba ya matumizi ya viungo (occupational therapist), mtaalamu wa kuzungumza (speech therapist), mtaalamu wa tiba ya mwili (physiotherapist), au daktari wa watoto) inayoelezea yafuatayo:
   - Haja ya vifaa vilivyoombwa
   - Jinsi vifaa vitakuza ustawi wa jumla wa mtoto, ukuaji na ushiriki katika shughuli za kila siku
   - Ushahidi wa majaribio ya kifaa (ikiwa yanafaa), ulio na tarehe ndani ya miezi sita ya maombi
3. **Beyi ya** vifaa vilivyoombwa
   - Sio zaidi ya miezi mitatu na halali katika mchakato wa tathmini.
4. Ikiwa mtoto wako ana **Ufadhili wa NDIS** toa yafuatayo:
   - Tambua ni kwa nini bidhaa/vipengee vilivyoombwa havijashughulikiwa na mpango wa NDIS wa mtoto
   - Uthibitisho wa kumalizika au kukataliwa kwa ufadhili wa NDIS
5. **Mapato ya Kaya (familia)** - Kwa kila mzazi/mlezi ambaye anawajibika kifedha kwa mtoto mambo yafuatayo lazima yawasilishwe:
   - **Taarifa** yako ya hivi majuzi ya Mapato ya ATO

KUONGEZA

- Ikiwa unapokea **Malipo ya Centrelink** - Taarifa yako ya Mapato ya Centrelink ya hivi majuzi
- Ikiwa mzazi/mlezi **ameajiriwa** - hati 2 za malipo (payslips) za hivi majuzi zaidi zinazoonyesha mapato ya mwaka
- Ikiwa mzazi/mlezi **hapokei Malipo ya Centrelink na hana kazi** - taarifa za benki za miezi 3 iliyopita.
- Ikiwa mzazi **amejiajiri** - taarifa za benki za miezi mitatu ya mwisho**.**

**Ikiwa wazazi wametengana na mmoja bado anachangia mahitaji ya mtoto (lakini anaishi nje ya kaya (familia)), hati (documentation) zao za kifedha zinahitajika pia.**

## Maombi

- Fomu ya maombi iko mtandaoni na iko kwa Kiingereza. Ikiwa unahitaji usaidizi wa kusoma na kuandika kwa Kiingereza, tafadhali tafuta usaidizi kutoka kwa mtu wa usaidizi kama vile mtaalamu wa matibabu, mfanyakazi wa kesi, mwalimu, mtoa tiba, mwanafamilia au rafiki.

## Maombi yasiyostahiki

- Mwombaji ametuma ombi la We Move Equipment Grant (Ruzuku ya Vifaa vya We Move) ndani ya miezi 12 iliyopita
- Ufadhili wa kurudi nyuma - gharama zinazotolewa tu baada ya idhini (approval) ya ruzuku ndizo zinazostahiki
- Vifaa visivyohusiana moja kwa moja na mahitaji ya ziada ya mtoto au si lazima kiafya
- Mbwa wa matibabu, mbwa wa msaada wa akili, na wanyama wa msaada wa kihemko (emotional)
- Gharama za usafiri
- Dhamana (warranties), bima, matengenezo, mikataba ya huduma, betri, matengenezo
- Ada za usimamizi au gharama za uendeshaji
- Vifaa vya michezo ambavyo havibadiliki au haieleweki jinsi vinavyosaidia mahitaji ya ziada
- Vifaa kutoka kwa wasambazaji wasio Waaustralia ambao hawawezi kutoa ankara (invoices) kwa Variety moja kwa moja
- Kazi kuu na gharama za ufungaji

## Uidhinishaji (approval) wa maombi ya ruzuku

- Maombi yanaidhinishwa na Kamati ya Ruzuku ya Variety. Arifa kupitia barua pepe inaweza kuchukua hadi wiki 8.

## Maombi ambayo yamefanikiwa

- Barua ya matokeo inatumwa kupitia barua pepe inayoonyesha jinsi ya kutumia ruzuku.
- Waombaji waliofaulu wana miezi 12 kutoka tarehe ya barua ya idhini (approval) ya kutumia ruzuku yao.
- Fedha ambazo hazijatumika zitachukuliwa baada ya tarehe ya kumalizika kwa ruzuku

## Malipo ya vifaa

- Mtoa huduma aliyebainishwa katika ombi lazima ampe mwombaji ankara ya kodi (tax invoice) itakayolipwa na Variety - The Children's Charity NSW/ACT kwa bidhaa na kiasi kilichoidhinishwa.
- Variety NSW/ACT haitoi pesa moja kwa moja kwa waombaji

## Maombi ambayo hayajafanikiwa

- Ni kwa uamuzi wa Kamati ya Ruzuku na inawezakana kutuma maombi tena baada ya miezi 12

**Taarifa zaidi**

Ikiwa unahitaji maelezo zaidi, tafadhali usisite kuwasiliana na timu ya Usaidizi kwa Watoto kwenye kidssupport@varietynsw.org.au